



MWAKA WA 101

28 Februari, 2020

TOLEO NA. 9

GAZETI

BEI SH. 1,000/=

LA

DODOMA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na
Kuandikishwa Posta kama
Gazeti

YALIYOMO

Taarifa ya Kawaida	Uk.	Taarifa ya Kawaida	Uk.
Kuthibitishwa Kazini	Na. 184 35	Tafsiri ya Kanuni za Huduma Ndogo za	
Notice <i>re</i> Supplement	Na. 185 35/7	Fedha (Majukumu ya Waziri)	Na. 202 42/56
Tanzia	37/8	Tangazo la Kufunga Kampuni	Na. 203-4 56
Kupotea kwa Hati ya Kumiliki Ardhi	Na. 186-93 38/40	Special Resolution	Na. 205-6 56/7
Kupotea kwa Leseni ya Makazi	Na. 194 40	Winding Up Resolution	Na. 207 57
Kupotea/Kuungua kwa Leseni ya Makazi ..	Na. 195 40	Business Registrations and Licensing	
Kupotea kwa Barua ya Toleo ya Kumiliki		Agency	Na. 208-9 57/8
Ardhi	Na. 196-8 41	Uthibitisho na Usimamizi wa Mirathi	Na. 210-1 58
Kampuni Iliyofutwa katika Daftari la		Change of Name by Deed Poll	Na. 212-3 58/9
Makampuni	Na. 199-200 41	Capital Markets and Securities Authority -	
Majina ya Wakaguzi wa Magari na		Tanzania	Na. 214 60/79
Watahini wa Madereva	Na. 201 42	Inventory of Unclaimed Property	Na. 215-7 87

KUTHIBITISHWA KAZINI

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 184

OFISI YARAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMANAUTAWALABORA

Kuwa Afisa Tawala Daraja la II kuanzia tarehe 01/07/2018

JAFARI Z. KALAGHE

TUNURA R. AMANI

Kuwa Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II kuanzia tarehe 01/07/2018

EDWIN M. KANJU

Kuwa Afisa Utumishi Daraja la II kuanzia tarehe 02/01/2019

LOVENESS J. CHOGA

Kuwa Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II kuanzia tarehe 02/01/2019

HASSAN Y. SHAIBU

MARIAM S. SADICK

MWANAHAWA M. MSUYA

Kuthibitishwa Kazini - (inaendelea tazama Ukurasa wa 87):-

Matangazo yahasuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika Gazeti. Yapelekwe kwa **Mhariri, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, S. L. P. 670. 40404 Dodoma, Simu za Ofisi: +255(026)2963630.** Kabla ya *Jumamosi ya kila Juma.*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 185

Notice is hereby given that Regulations, Order, Notices and Kanuni as Set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 9 dated 28th February, 2020 to this number of the *Gazette*:-

Regulations under the Mining (Importation of Minerals for Mineral and Gem Houses) (Amendment) (Government Notice No. 136 of 2020).

Regulations under the Tobacco Industry Licensing Fees (Amendments) (Government Notice No. 137 of 2020).

Order under the Executive Agencies (e-Government Agency) (Disestablishment) (Government Notice No. 138 of 2020).

Order under the Criminal Procedure (Appontment of Hand Writing Expert) (Government Notice No. 139 of 2020).

Notice under the General Laws Revision (Government Notice No. 140 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 141 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 142 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 143 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 144 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 145 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 146 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 147 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 148 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 149 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 150 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 151 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 152 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 153 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 154 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 155 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 156 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 157 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 158 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 159 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 160 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 161 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 162 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 163 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 164 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 165 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 166 of 2020).

Notice under the National Prosecutions Services (Appontment of Public Prosecutors) (Government Notice No. 167 of 2020).

Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Majukumu ya Waziri) (Tangazo la Serikali Na. 168 la mwaka 2020).

Regulations under the Tax Administration (General) (Amendment) (Government Notice No. 169 of 2020).

Order under the Income Tax (Exemption) (Capital Gains and Gains or Losses from Realization of Assts or Liabilities) (Government Notice No. 170 of 2020).

Order under the Income Tax (Exemption) (Chargeable Income and Tax Payable) (Government Notice No. 171 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Supply and Installation of Four New 400KV Substations at Iringa, Dodoma, Singida and Shinyanga) (Backbone Transmission Investment Project) (BTIP)-Lot T6-2) (KEC International Ltd) (Amendment) (Government Notice No. 172 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Provision of Consultancy for Preparation of Catchment Conservation Plans in Nine Basin and Implementation in Wami/Ruvu Basin-Tanzania) (M/S GEO Network Limited in Joint Venture with M/S Witek Company and Ltd M/S EWM Consult Tanzania Ltd) (Government Notice No. 173 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Roads and Bridges Projects Funded by the Government of United Republic of Tanzania) (Construction, Repair and Maintenance of Roads and Bridges) (Tanzania Roads Agency (TANROADS)) (Government Notice No. 174 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Construction of Pumped Water Supply Scheme for Kalamba Juu Village, Kondo District Council in Dodoma Region) (M/S Flying Construction Company Limited, Building and Civil Engineers) (Government Notice No. 175 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Construction of Pumped Water Supply Scheme for Mtiryangwi Village, Kondo District Council in Dodoma Region) (M/S Mushi Brothers Investment Ltd) (Government Notice No. 176 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Construction of Pumped Water Supply Scheme for Haire Village, Kondo District Council in Dodoma Region) (M/S Nyakire Investment Limited) (Government Notice No. 177 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Construction of Pumped Water Supply Scheme for Mwembeni Village, Kondo District Council in Dodoma Region) (M/S TS Solutions (T) Ltd and Shamoka Building & Civil Constructors Ltd JV) (Government Notice No. 178 of 2020).

Order under the Value Added Tax (Exemption) (Construction of Gravity main, Distribution Pipelines and Storage Reservoir for Pugu and Gongo la Mboti Area) (M/S China Henan International Group (CHICO)) (Government Notice No. 179 of 2020).

TANZIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **S'SGT ANDERSON ELIAMIN MBAGA** kilichotokea tarehe 25/07/2019 kwa Ajali ya Gari kijiji cha Mvomero.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **SGT ALFRED ARON KANDONGA** kilichotokea tarehe 15/08/2019 kwa Shinikizo la Damu, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **ASP JAFFARY ALLY MCHOCHO** kilichotokea tarehe 21/08/2019 kwa Ugonjwa, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **CPL KHADIJA AYUBU** kilichotokea tarehe 26/08/2019 kwa Kugongwa na Gari Kisarawe.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **CPL HIDAYA NKAILOTE SHANTIWA** kilichotokea tarehe 27/08/2019 kwa Ugonjwa Hospitali ya Mkoa wa Songwe.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **S'DGT ELINEEMA MARTIN MAHIMBA** kilichotokea tarehe 31/08/2019 Hospitali ya Morogoro.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **S'SGT YAHAYA DANIEL MKOGA**

kilichotokea tarehe 31/08/2019 kwa Ugonjwa Hospitali ya Muhimbili Dar es Salaam.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **WDR BRIGHT C. MWAKAHABALA** kilichotokea tarehe 03/09/2019 katika Hospitali Teule ya Uwata Mbeya.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **ASP PETER DAMAS MBELE** kilichotokea tarehe 08/09/2019 kwa Ugonjwa Hospitali ya Sokoine Mkoani Lindi.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **CPL MHINA FRANCIS MHINA** kilichotokea tarehe 24/10/2019 kwa Kupigwa Risasi na Majambazi Mbezi Beach Dar es Salaam.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **S'SGT DANIEL MICHAEL MAPUNDA** kilichotokea tarehe 15/11/2019 kwa Ajali ya Gari Eneo la Mikese Morogoro.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha **NDUGU NUHU AHMED MWASUMILWE** aliyekuwa Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya Mpango na Uratibu kilichotokea tarehe 23/12/2019 Dar es Salaam na kuzikwa nyumbani kwao Mkoani Njombe tarehe 24/12/2019.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 186

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 175927.

Miliki aliyeandikishwa: DANIEL JAMES MIKENZE WA S. L. P. 35972, KINONDONI DAR ES SALAAM.

Ardhi: Kiwanja Na. 25 Kitalu Na. 2 Makongo, Kinondoni.

Muombaji: DANIEL JAMES MIKENZE WA S. L. P. 35972 KINONDONI DAR ES SALAAM.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
7 Januari, 2020

BRENDA KURINGE,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 187

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 54069.

Miliki aliyeandikishwa: TANZANIA LEGAL CORPORATION, 2203.

Ardhi: Kiwanja Na. 649 Kitalu Na. F Msasani, Kinondoni.

Muombaji: THE OFFICE TREASURY REGISTRAR WA S. L. P. 3193 KINONDONI DAR ES SALAAM.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
13 Februari, 2020

APOLLO LAIZER,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 188

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Usajili wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 4404.

Miliki aliyeandikishwa: DEVOTA JACOB MAYUYA WA S. L. P. 132, MWANZA.

Ardhi: L. O. No. 116161, Kiwanja Na. 11 Kitalu 'B' Igoma Mwanza Manispaa

Muombaji: DEVOTA JACOB MAYUYA WA S. L. P. 132 MWANZA.

Eneo: 600 mita za Mraba.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi cho chote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe Ofisi ya Msajili wa Hati, S. L. P. 1101, Mwanza.

Mwanza,
16 Januari, 2020

IVAN AMURIKE,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 189

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Usajili wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 11619.*Mmiliki aliyeandikishwa:* OLASITI INVESTMENT CO. LTD WA S. L. P. 10275, ARUSHA.*Ardhi:* Na. 163286, Kiwanja Na. 176 Kitalu 'E' Igoma Mwanza Manispaa.*Muombaji:* OLASITI INVESTMENT CO. LTD WA S. L. P. 10275, ARUSHA.*Eneo:* 486 mita za Mraba.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi cho chote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe Ofisi ya Msajili wa Hati, S. L. P. 1101, Mwanza.

Mwanza,
22 Novemba, 2019

IVAN AMURIKE,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 190

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 253-DLR.*Mmiliki aliyeandikishwa:* ABDUL KIKOO WA S. L. P. 105 DODOMA.*Ardhi:* Kiwanja Na. 292 Kitalu '-' Makole Dodoma.*Muombaji:* ABDUL KIKOO WA S. L. P. 400 DODOMA.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1249, Dodoma.

Dodoma,
13 Desemba, 2019

G. W. MAUYA,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 191

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 112847.*Mmiliki aliyeandikishwa:* CANDIDA AMANI NGOWI.*Ardhi:* Kiwanja Na. 48 Kitalu '27 Buyuni Halmashauri ya Ilala.*Muombaji:* CANDIDA AMANI NGOWI WA S. L. P. 1204, DAR ES SALAAM.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
30 Januari, 2020

JOANITHA KAZINJA,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 192

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 182406.*Mmiliki aliyeandikishwa:* MUNA OMAR BAWAZIR.*Ardhi:* Kiwanja Namba 162 Block 23 Gezaulole.*Muombaji:* MUNA OMAR BAWAZIR WA S. L. P. 36190, DAR ES SALAAM.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi cho chote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
17 Februari, 2020

APOLLO E. LAIZER,
Msajili wa Hati Msaidizi Mwandamizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 193

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Nambari: 85106.

Mmiliki aliyeandikishwa: JAPHET MBOTO MAKAU WA S. L. P. 78783, DAR ES SALAAM.

Ardhi: Kiwanja Na. 140 Kitalu 'C' Kilimanjaro, Manispaa ya Morogoro.

Muombaji: JAPHET MBOTO MAKAU WA S. L. P. 78783, DAR ES SALAAM.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi cho chote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 2637, Morogoro.

Morogoro,
25 Februari, 2020

SILVERIUS PETER QORRO,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 194

LOSS OF CERTIFICATE OF TITLE
The Land Registration Act
(Cap. 334)

Certificate of Title: 139170.

Registered Owner: NAJIM ZUBER MSENDA OF P. O. BOX ..., KINONDONI DAR ES SALAAM.

Land: Plot No. 106 Block X at Goba, Ubungo

Applicant: NAJIM ZUBER MSENDA OF P. O. BOX, KINONDONI, DAR ES SALAAM.

TAKE NOTICE that the Certificate of Title to the land described above is said to be lost and that I intend to issue new Certificate of Title in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within one month from the date this Notice is published in the Official *Gazette*.

THE ORIGINAL CERTIFICATE OF TITLE if found, should be delivered at the Land Registry of P. O. Box 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
14 Februari, 2020

APOLLO LAIZER,
Assistant Registrar of Title

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 195

KUPOTEA KWA LESENI YA MAKAZI
Sheria ya Usajili wa Nyaraka
(Sura 117)

Leseni Nambari: TMK036555.

Mmiliki aliyeandikishwa: SOPHIA MIRAJI FUNDI.

Namba ya Eneo la Ardhi: TMK/MBGK/KJC24/34.

Mwombaji: SOPHIA MIRAJI FUNDI.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba leseni ya makazi tajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Nakala ya Leseni ya Makazi iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa siku ishirini na nane (28) tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali. Na isitumike kwa Dhamana ya aina yo yote ile.

LESENI YA MAKAZI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Nyaraka Msaidizi, S. L. P. 46343 Temeke, Dar es Salaam.

E. R. PALLANGYO,
Msajili Msaidizi wa Nyaraka
Manispaa ya Temeke

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 196

KUPOTEA/KUUNGUA KWA LESENI YA MAKAZI
Sheria ya Usajili wa Nyaraka
(Sura 117)

Namba ya Usajili: 203625.

Leseni Nambari: TMK044927.

Mmiliki aliyeandikishwa: MUZDALIFA NUHU YASIN.

Namba ya Eneo la Ardhi: TMK/CHB/MNZ16/162.

Muombaji: MUZDALIFA NUHU YASIN.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba leseni ya makazi tajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Nakala ya Leseni ya Makazi iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa siku ishirini na nane (28) tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali. Na isitumike kwa Dhamana ya aina yo yote ile.

LESENI YA MAKAZI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Nyaraka Msaidizi, S. L. P. 46343 Temeke, Dar es Salaam.

E. R. PALLANGYO,
Msajili Msaidizi wa Nyaraka
Manispaa ya Temeke

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 197

KUPOTEAKWABARUA YA TOLEO YAKUMILIKI
ARDHI*Sheria ya Umiliki wa Ardhi ya Mwaka 1999**Barua ya Toleo Kumb. Na.: LD/TM/O/1.**Mmiliki aliyeandikishwa: HUSSEIN SAID MBWERA.**Ardhi: Kiwanja Na. 122 Kitalu 'M' Eneo la Temeke Manispaa ya Temeke Jijini Dar es Salaam.*

TAARIFA INATOLEWA kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika Gazeti la Serikali.

BARUA HALISI YA TOLEO ikipatikana, irudishwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke S. L. P. 46343 Dar es Salaam.

P. A. MASOY,
*Afisa Ardhi Mteule
Manispaa ya Temeke*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 198

KUPOTEAKWABARUA YA TOLEO YAKUMILIKI
ARDHI*Sheria ya Umiliki wa Ardhi ya Mwaka 1999**Barua ya Toleo Kumb. Na.: DCC/LD/59538/CY.**Mmiliki aliyeandikishwa: ACHERU OMARY KAGELWA WA S. L. P. 18042, DAR ES SALAAM.**Namba ya Kiwanja: 472 Kitalu 'B' Kinyerezi.**Mwombaji: ACHERU OMARY KAGELWA WA S. L. P. 18042, DAR ES SALAAM.*

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Barua ya Toleo ya Kiwanja kilichotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **Barua ya Toleo** mpya badala yake, iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tangu tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

BARUA YA TOLEO YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa Afisa Ardhi Mteule, Manispaa ya Ilala, S. L. P. 20950 Dar es Salaam.

FURAHA MWAKAPALILA,
*Kny: Mkurugenzi wa Manispaa
Halmashauri ya Manispaa ya Ilala*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 199

KUPOTEAKWABARUA YA TOLEO YAKUMILIKI
ARDHI*Sheria ya Umiliki wa Ardhi ya Mwaka 1999**Barua ya Toleo Kumb. Na.: LD/TM/MBG/G/52.**Mmiliki aliyeandikishwa: KILAKA TUPA.**Ardhi: Kiwanja Na. 52 Kitalu 'G' Eneo la Mbagala Manispaa ya Temeke Jijini Dar es Salaam.*

TAARIFA INATOLEWA kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika Gazeti la Serikali.

BARUA HALISI YA TOLEO ikipatikana, irudishwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke S. L. P. 46343, Dar es Salaam.

P. A. MASOY,
*Afisa Ardhi Mteule
Manispaa ya Temeke*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 200

KAMPUNI ILIYOFUTWA KATIKA DAFTARI LA
MAKAMPUNI*Sheria ya Makampuni
(NA. 12 YA 2002)*

Inatolewa Ilani chini ya kifungu cha 400(5) cha Sheria ya Makampuni kwamba Kampuni ifuatayo imefutwa katika daftari la Makampuni tokea tarehe ya ilani hii.

JOSEPH DIDAS AMBROCE LIMITED

S. KASERA,
Msajili Msaidizi Mkuu wa Makampuni

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 201

KAMPUNI ILIYOFUTWA KATIKA DAFTARI LA
MAKAMPUNI*Sheria ya Makampuni
(NA. 12 YA 2002)*

Inatolewa Ilani chini ya kifungu cha 400(5) cha Sheria ya Makampuni kwamba Kampuni ifuatayo imefutwa katika daftari la Makampuni tokea tarehe ya ilani hii.

PUNAMANI LIMITED

S. KASERA,
Msajili Msaidizi Mkuu wa Makampuni

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 202

ORODHA YA MAJINA YA WAKAGUZI WA MAGARI NA WATAHINI WA MADEREVA
(VEHICLE INSPECTION AND DRIVER EXAMINER)

NA.	<i>JINA NA CHEO</i>	<i>FANI ALIYOSOMEA</i>	<i>KIWANGO</i>	<i>CHUO ALICHOSOMEA</i>
1.	G 795 PC FRANCIS MAGINGO SHANGO	VEHICLE INSPECTION AND DRIVER EXAMINER	CHETI	NIT
2.	WP 4954 CPL MODESTA GABRIEL BUSUGU	VEHICLE INSPECTION AND DRIVER EXAMINER	CHETI	NIT
3.	WP 4371 CPL JULIANA FULLA IBALAJA	VEHICLE INSPECTION AND DRIVER EXAMINER	CHETI	NIT

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 203

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA
(SURA YA 407)

TAFSIRI YA KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (MAJUKUMU YA WAZIRI) ZA MWAKA 2019

Toleo hili la Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Majukumu ya Waziri) za Mwaka 2019, Tangazo la Serikali Na. 575 la tarehe 2 Agosti, 2019, ni Tafsiri rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria mbalimbali, Sura ya 1.

TANGAZO LA SERIKALI NA. 575 LA TAREHE 2/8/2019

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA
(SURA 407)

KANUNI

(Zimeandaliwa chini ya kifungu cha 15(4))

KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (MAJUKUMU YA WAZIRI) ZA MWAKA 2019

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina la kanuni na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YAPILI

A: URATIBU WA BIAHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

4. Uratibu wa biashara ya huduma ndogo ya fedha.
5. Uteuzi wa mratibu.
6. Majukumu ya mratibu.
7. Uundaji wa kamati.

8. Majukumu ya kamati.
9. Jukwaa la wadau wa huduma ndogo za fedha.
10. Malengo ya Jukwaa.

B: UBADILISHANAJI WA TAARIFA ZINAZOHUSU BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

11. Ubadilishanaji wa taarifa.
12. Uhitaji wa taarifa.
13. Ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa wadau.

SEHEMU YA TATU

UHAMASISHAJI WA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

14. Uhamasishaji wa biashara ndogo za fedha.
15. Usajili wa wahamasishaji.
16. Hati ya usajili.
17. Kukataliwa kwa maombi ya usajili.
18. Rejesta ya wahamasishaji.
19. Kufuta usajili wa mhamasishaji.
20. Kibali kwa wahamasishaji.
21. Utoaji wa miongozo.

SEHEMU YANNE

MASHARTI YA JUMLA

22. Uzingatiaji wa utawala bora.
23. Rufaa.
24. Kamati ya rufaa.
25. Ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja.
26. Makosa na adhabu.

—————
MAJEDWALI
—————

Tangazo la Serikali Na. 575 (linaendelea)

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA
(SURA 407)

KANUNI

(Zimeandaliwa chini ya kifungu cha 15(4))

KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (MAJUKUMU YA WAZIRI) ZA MWAKA 2019

SEHEMU YAKWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina la
kanuni na
tarehe ya
kuanza
kutumika

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Majukumu ya Waziri) za Mwaka 2019 na zitaanza kutumika tarehe ambayo Waziri atatangaza kupitia taarifa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa biashara ya huduma ndogo za fedha zinazofanywa chini ya Daraja la 2, Daraja la 3 na Daraja la 4.

Tafsiri
Sura
407 Sura
197

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa maktadha ukihitaji vinginevyo-
 “Sheria” maana yake ni Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha;
 “Benki” maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;
 “Mtumiaji” itakuwa na maana iliyotolewa katika Sheria;
 “Mamlaka Kusimishwa” itakuwa na maana iliyotolewa katika Sheria;
 “mratibu” maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini y akanuni ya 5 na atakuwa na jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu sekta ndogo ya fedha;
 “Jukwaa” maana yake ni jukwaa la wadau wa huduma ndogo za fedha lililoanzishwa chini ya kanuni ya 9(1);
 “mamlaka ya serikali za mitaa” itakuwa na maana iliyotolewa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) au Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);
 “watoa huduma ndogo za fedha” itakuwa na maana iliyotolewa katika Sheria;
 “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha;
 “Wizara” maana yake ni Wizara ya Fedha;
 “mhamasishaji” maana yake ni mtu binafsi au taasisi iliyosajiliwa chini ya Kanuni hizi kwa ajili ya kuhamasisha biashara ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa kanuni ya 16;
 “uhamasishaji” maana yake ni uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha unaorejewa chini ya kanuni ya 14;
 “Waziri husika” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya ushirika au kama inavyoweza kuwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya mamlaka ya serikali za mitaa;
 “mdau” maana yake ni mtu binafsi au taasisi ambayo inajishughulisha moja kwa moja au kwa namna nyingine na shughuli zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha na inajumuisha watoa huduma ndogo za fedha, watumiaji, wahamisishaji na taasisi za serikali.

Sura 287
na
288

SEHEMU YA PILI

C: URATIBU WA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Uratibu
wa
biashara
ya
huduma
ndogo za
fedha

4.-(1) Waziri anaweza, kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake ya kuweka mazingira wezeshi, endelevu na uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha, kuweka utaratibu wa kuratibu shughuli zote zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha.

(2) Waziri anaweza, kwa madhumuni ya uratibu wa shughuli zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha na baada ya mashauriano na Mawaziri husika, kuhakikisha:

- (a) uteuzi wa waratibu kutoka katika kila mamlaka ya serikali za mitaa na wizara husuka unafanyika;
- (b) uanzishwaji wa Jukwaa la Wadau wa Huduma Ndogo za Fedha ili kujadili masuala yanayohusu sekta ndogo ya fedha; na
- (c) uundaji wa kamati za kushauri utekelezaji wa Sheria.

5.-(1) Kutakuwa na mratibu atakayeteuliwa na mamlaka ya uteuzi katika Wizara yenye dhamana na mamlaka ya serikali za mitaa na kila mamlaka ya serikali za mitaa. Uteuzi wa mratibu

(2) Mratibu atakuwa ni mtu mwenye sifa na uzoefu katika masuala yanayohusu uchumi, fedha, maendeleo ya jamii, ujasiliamali, usimamizi wa biashara au fani nyingine yo yote inayoendana na hizo.

6.-(1) Mratibu aliyeteuliwa chini ya kanuni ya 5(1) atakuwa na wajibu wa uratibu wa masuala yote yanayohusu biashara ya huduma ndogo za fedha katika eneo lake

Maju-kumu ya mratibu

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mratibu atakuwa na wajibu wa:

- (a) kutengeneza na kusimamia kanunizi za huduma ndogo za fedha katika eneo lake;
- (b) kuhamasisha biashara ya huduma ndogo za fedha nchini;
- (c) kufuatilia na kutathmini maendeleo ya biashara ya huduma ndogo za fedha;
- (d) kufanya usajili wa wahamasishaji na kutoa vibali kwa wahamasishaji;
- (e) kusajili na kufuta usajili wa wahamasishaji;
- (f) kuhakikisha wahamasishaji wanazingatia kanuni na miongozo iliyoandaliwa chini ya Kanuni hizi;
- (g) kuandaa na kuwasilisha taarifa za vipindi mbalimbali za huduma ndogo za fedha kwa Waziri kwa vipindi mbalimbali katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza; na
- (h) kutekeleza kazi nyingine kama itakavyohitajika kwa madhumuni ya uratibu wa biashara ya huduma ndogo za fedha.

(3) Taarifa za vipindi mbalimbali zinazoandaliwa na mratibu chini ya kanuni ndogo ya 2(e) zitajumuisha maendeleo ya shughuli zote zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha na zitatakiwa:

- (a) kwa shughuli zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 2, ziwasilishwe kwa Wizara;
- (b) kwa shughuli zinazohusu biashara za huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 3, ziwasilishwe kwa Wizara kupitia Wizara yenye dhamana na masuala ya ushirika; na
- (c) kwa shughuli zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 4, ziwasilishwe kwa Wizara kupitia Wizara yenye dhamana na masuala ya mamkaka ya serikali za mitaa.

(4) Baada ya kupokea taarifa kutoka mamlakea husika wanapaswa, kwa kuzingatia idhini kutoka mamkala husika, kuwasilisha taarifa kwa Wizara.

7.-(1) Wazira anaweza kuunda kamati kwa madhumuni ya kumshauri kuhusu uratibu wa biashara ya huduma ndogo za fedha na utekelezaji wa masharti ya Sheria.

Uundaji wa kamati

(2) Kamati inayoundwa chini ya kanuni ndogo ya (1) inaweza kujumuisha wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi tisa watakaoteuliwa kutoka miongoni mwa wadau husika.

8. Majukumu ya Kamati yatajumuisha yafuatayo:

Maju-kumu ya kamati

- (a) kubainisha changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya fedha na kupendekeza suluhisho;
- (b) kubainisha ubunifu katika biashara ya huduma ndogo za fedha kwa madhumuni ya kuendeleza sekta ndogo ya fedha;
- (c) kufanya mapitio ya masuala yatakayojitokeza katika biashara ya huduma ndogo za fedha;
- (d) kujadili masuala ya sera na sheria katika biashara ya huduma ndogo za fedha;
- (e) kuchambua mapendekezo ya Jukwaa na kumshauri Waziri kwa ajili ya utekelezaji bora; na
- (f) kujadili masuala mengine yo yote yanayohusu sekta ndogo ya fedha.

9.-(1) Kutakuwa na jukwaa litakalojulikana kama Jukwaa la Wadau wa Huduma Ndogo za Fedha litakalojadoli masuala yenye maslahi ya pamoja kwa madhumuni ya uratibu na uendelezaji wa sekta ndogo ya fedha.

Jukwaa la wadau wa huduma ndogo za fedha

(2) Jukwaa litajumuisha wawakilishi kutoka:

- (a) Wizara;

- (b) Wizara husika;
- (c) Benki;
- (d) Mamlaka Kasimishwa;
- (e) Watoa huduma ndogo za fedha;
- (f) jumuiya za watoa huduma ndogo za fedha;
- (g) watoa huduma ya uendelezaji wa biashara;
- (h) washirika wa maendeleo;
- (i) wahamasishaji; na
- (j) wadau wengine wote kama itakavyoamuliwa na Wizara.

(3) Jukwaa litaitishwa angalau mara moja katika mwaka wa kalenda au kwa kipindi kisichozidi mezi 15 baada ya Jukwaa lililopita.

- (4) Wizara itakuwa na wajibu wa kuitisha mikutano ya Jukwaa.
- (5) Gharama zinazohusu Jukwaa zitagharamiwa na wajumbe.
- (6) Jukwaa litaweke taratibu za uendeshaji wa mikutano yake.

Malengo
ya
Jukwaa

10. Malengo ya Jukwaa yatakuwa ni:
- (a) kubainisha changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya fedha na kupendekeza suluhisho;
 - (b) kubainisha na kuhamasisha ubunifu katika sekta ndogo ya fedha;
 - (c) kuchambua masuala yanayojitokeza katika biashara ya huduma ndogo za fedha na kupendekeza hatua stahiki;
 - (d) kujadili masuala ya sera na sheria yanayohusu sekta ndogo ya fedha na kupendekeza suluhisho; na
 - (e) kujadili na kutatua masuala mengine yanayohusu sekta ndogo ya fedha.

D. UBADILISHANAJI WA TAARIFA ZINAZOHUSU BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Ubadili-
shanaji wa
taarifa

11.-(1) Waziri anaweza, kuwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria, kubadilishana taarifa zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha na Mawaziri husika.

- (2) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Mawaziri husika, kupewa taarifa au nyaraka kw amadhumuni ya-
 - (a) kuwezesha utekelezaji wa Sheria;
 - (b) kutathmini hali ya biashara ya huduma ndogo za fedha;
 - (c) ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha; na
 - (d) kukusanya na kusambaza taarifa zinazohusu sekta ndogo ya fedha.

- (3) Taarifa za kubadilishana zinaweza kujumuisha:
 - (a) masuala yanayojitokeza katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha;
 - (b) matokeo ya utafiti katika biashara ya huduma ndogo za fedha;
 - (c) maendeleo ya hali ya biashara ya huduma ndogo za fedha; na
 - (d) taarifa nyingine husika kama zitakavyohitajika kwa madhumuni ya Sheria.

(4) Taarifa zitakazotolewa na Waziri chini ya Kanuni hizi zitakuwa za siri, isipokuwa kama itakavyohitajika vinginevyo kwa mujibu wa Sheria ya Bunge.

(5) Mawaziri husika wanapaswa, baada ya mashauriano na Waziri, kutoa taarifa kwa umma kuhusu masuala ya biashara ndogo ya fedha.

Uhitaji wa
taarifa

12.-(1) Waziri anaweza, kwa dhumuni la utekelezaji wa Sheria, kuhitaji kwa maandishi taarifa zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha na kuainisha kipindi ambacho taarifa hizo zinapaswa kutolewa kutoka kwa mdau.

(2) Mdau atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha pale itakapohitajika.

- (3) Mtu ye yote atakayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (2) anatenda kosa.

13.-(1) Wadau wanaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli ya huduma ndogo za fedha, kubadilishana miongoni mwao taarifa zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha.

Ubadili-
shanaji wa
taarifa
miongoni
mwa
wadau

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), taarifa zitakazotolewa kwa wadau zinaweza kujumiusha:

- (a) uzoefu na maendeleo ya biashara su sekta ndogo ya fedha;
- (b) masuala yanayojitokeza katika biashara ya huduma ndogo za fedha;
- (c) fursa au changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya fedha;
- (d) masuala ya ubunifu katika biashara ya huduma ndogo za fedha; na
- (e) taarifa nyingine yo yote husika.

(3) Taarifa zitakazotolewa miongoni mwa wadau zinaweza kutolewa kupitia:

- (a) tovuti rasmi;
- (b) mikutano ya wadau au Jukwaa;
- (c) magazeti;
- (d) vyombo vya habari vya kijamii; au
- (e) njia nyingine zo zote za mawasiliano.

(4) Wadau watahakikisha kuwa taarifa zitakazotolewa ni sahihi.

(5) Kwa kuzingatia kanuni hii, mtu ambaye kwa kukusudia au kwa kufahamu, anatoa au kusambaza taarifa zisizo sahihi au za uongo, anatenda kosa.

SEHEMU YA TATU

UHAMASISHAJI WA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

14.-(1) Bila ya kuathiri masharti husika ya Sheria, uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha utafanywa na wahamasishaji waliosajiliwa chini ya Kanuni hizi.

Uhamasi-
shaji wa
biashara
ya
huduma
ndogo za
fedha

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha zhini ya Kanuni hizi utajumuisha shughuli yo yote inayofanywa na mhamasishaji inakusudia:

- (a) kusaidia uanzishwaji au uendeshaji wa mtoa huduma ndogo za fedha; au
- (b) kutoa mafunzo na elimu ya fedha kwa watoa huduma ndogo za fedha, watumiaji au wadau wengine; au
- (c) kutoa msaada kwa mtoa huduma ndogo za fedha utakaomwezesha kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha kwa ufanisi.

(3) Kwa madhumuni ya kuhakikisha uendelezaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha, Waziri anaweza:

- (a) kuhakikisha uwepo wa mazingira wezeshi kwa wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha;
- (b) kuhimiza utafiti na maendeleo katika sekta ndogo ya fedha;
- (c) kujenga uwezo endelevu katika sekta ndogo ya fedha;
- (d) kuhimiza ubunifu;
- (e) kuhamasisha vikundi vya jamii vya huduma ndogo za fedha kujiunga na mfumo rasmi wa kifedha; na
- (f) kufanya utafiti kuhusu biashara ya huduma ndogo za fedha.

15.-(1) Mtu hatafanya uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha pasipo kusajiliwa kama mhamasishaji.

Usajili wa
wahama-
sishaji

(2) Mtu anayetaka kufanya uhamasishaji wa biashara ndogo za fedha anapaswa kuomba usajili kwa mamlaka ya serikali za mitaa.

(3) Mambi ya usajili chini ya kifungu kidogo cha (2), yatakuwa katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na yataambatana na yatuatayo:

- (a) barua ya utambulisho au idhini kutoka kwa mamlake husika;
- (b) hati ya usajili au uanzishwaji kutoka kwenye mamlaka husika;
- (c) ada isiyorejeshwa itakayoainishwa ambayo haitazidi fedha za Kitanzania shilingi elfu hamsini; na
- (d) taarifa au nyaraka nyingine zo zote husika kama zitakavyohitajika na mamlaka ya serikali za mitaa.

- Hati ya usajili 16.-(1) Mamlaka ya serikali za mitaa inaweza, ikiwa itaridhika na maombi yaliyofanywa chini ya kanuni ya 15, kutoa hati ya usajili kwa mhamasishaji.
- (2) Hati ya usajili iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itakuwa katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na itakuwa na vigezo na masharti mahsusi yatakayozingatiwa na mhamasishaji.
- (3) Pamoja na vigezo na masharti chini ya kanuni ndogo ya (2), mhamasishaji atazingatia vigezo na masharti kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.
- (4) Hati ya usajili inayotolewa chini ya kanuni hii itakuwa halali kwa kipindi cha miaka wiwili na inaweza kuhuishwa.
- Kukataliwa kwa maombi ya usajili 17.-(1) Mamlaka ya serikali za mitaa inaweza, pale ambapo haijaridhika na maombi yaliyowasilishwa chini ya kanuni ya 15, kukataa maombi ya usajili na itamjulisha muombaji ipasavyo.
- (2) Muombaji ambaye maombi yeke yamekataliwa anaweza kuomba upwa, ikiwa kasoro zilizosababisha kukataliwa kwa maombi ya awali au mengine yaliyofuatia zimesahihishwa au vinginevyo kutatuliwa.
- Rejesta ya wahamasishaji 18.-(1) Kutakuwa na Rejesta ya wahamasishaji wote wa biashara ya huduma ndogo za fedha katika kila mamlaka ya serikali za mitaa.
- (2) Taarifa za Rejesta zitapatikana kwa umma baada ya malipo ya ada ya shilingi za Kitanzania elfu tano.
- (3) Rejesta itakuwa na taarifa zifuatazo:
- maelezo ya mhamasishaji yatakayojumuisha jina na anwani;
 - hadhi ya kisheria ya mhamasishaji;
 - aina ya huduma za uhamasishaji;
 - eneo la uendeshaji; na
 - taarifa nyingine kama zitakavyohitajika kwa dhumuni la usajili.
- Kufuta usajili wa mhamasishaji 19.-(1) Mamlaka ya serikali za mitaa inaweza, kufuta usajili wa mhamasishaji kwenye Rejesta, iwapo itajiridhisha kwamba:
- mhamasishaji ameshindwa kuzingatia vigezo na masharti ya usajili;
 - mhamasishaji ameshindwa kuzingatia miongozo itakayotolewa;
 - hati ya usajili au uanzishwaji imefutwa na Mamlaka husika;
 - mhamasishaji amepatikana na hatia ya makosa yanayohusu biashara ya huduma ndogo za fedha; au
 - mhamasishaji anajihusisha na vitendo vibaya ambavyo vinaathiri maadili na ustawi wa biashara ya huduma ndogo za fedha.
- (2) Bila ya kujali matakwa ya kanuni ndogo ya (1), mhamasishaji aliyekiuka masharti atapewa notisi ya siku 30 ili atoe maelezo ya sababu za kutofuatiwa usajili.
- Kibali cha wahamasishaji 20.-(1) Mhamasishaji anayekusudia kufanya biashara ya uhamasishaji katika eneo tofauti na mamlake ya serikali za mitaa ambayo amesajiliwa ataomba kibali cha kufanya uhamasishaji katika eneo husika.
- (2) Maombi ya kibali kinachotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) yanapaswa kuwasilishwa kwa mratibu yakiambatana na:
- barua ya maombi;
 - nakala ya hati halali ya usajili iliyohibitishwa;
 - ada ya maombi isiyorejeshwa ya shilingi za Kitanzania elfu kumi; na
 - taarifa au nyaraka nyingine husika kama zitakavyohitajika.
- (3) Mratibu, baada ya kujiridhisha na maombi yaliyofanywa chini ya kanuni ndogo ya (2), atatoa barua ya kibali kwa mhamasishaji kuendesha shughuli zake katika eneo husika.
- Utoaji wa miongozo 21.-(1) Waziri anaweza, kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa Kanuni hazi, kutoa miongozo ya jumla au mahsusi inayohusu ustawi, uratibu na uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha.

(2) Waziri anaweza kufanya mapitio ya miongozo mara kwa mara kadri itakavyohitajika.

SEHEMU YANNE
MASHARTI YA JUMLA

22.-(1) Kila mtoa huduma ndogo za fedha atazingatia misingi ya utawala bora ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na utoaji wa taarifa.

Uzinga-
taji wa
utawala
bora

(2) Menejimenti ya mtoa huduma ndogo za fedha itaundwa na watu wenye mienendo inayokubalika na uadilifu ambao wanatekeleza majukumu yao kwa maono na ustadi wa maslahi ya wanachana au wateje wake.

23.-(1) Mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Benki au Mamlaka Kasimishwa uliotolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria anaweza, ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya uamuzi, kukata rufaa kwa Waziri.

Rufaa

(2) Mtu anayekusudia kukata rufaa kwa Waziri kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), atawasilisha rufaa yake kwa maandishi kwa Waziri itakayoainisha:

- (a) chimbuko la rufaa yake;
- (b) sababu za rufaa yake; na
- (c) masuala mengine yo yote husika.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), Waziri ndani ya siku thelathini rangu tarehe ya kupokea rufaa, ataamua rufaa hiyo.

(4) Katika kuamua rufaa chini ya kifungu kidogo cha (3), Waziri anaweza kumtaka mkata rufaa:

- (a) kutoa taarifa zote muhimu na nyaraka ambazo ndozo msingi wa rufaa yake; au
- (b) kufika mbele ya Waziri au kamati.

(5) Endapo mkata rufaa atahitajika mbele ya Waziri au Kamati, mkata rufaa huyo atakuwa na haki ya kuwakilishwa.

(6) Uamuzi wa Waziri utatolewa kwa maandishi.

(7) Mtu ye yote ambaye hararidhishwa na uamuzi wa Waziri, anaweza kutafuta haki kwenye mahakama yenye mamlaka husika.

24.-(1) Waziri anaweza, kwa madhumuni ya rufaa na pale atakapoona inafaa, kuunda kamati ya kutoa ushauri huhusu rufaa.

Kamati
ya rufaa

(2) Kamati iliyoteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1), itaundwa na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano wenye uadilifu na weledi katika taaluma husika watakaoteuliwa kutoka Wizara au taasisi nyingine husika.

25.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, Benki au Mamlaka Kasimishwa itahakikisha kila mtoa huduma ndogo za fedha anaweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya wateja.

Ushughu-
likiaji wa
malala-
miko ya
wateja

(2) Malalamiko yote ya wateja yatashughulikiwa kwa namna itakayoainishwa katika utaratibu wa kushughulikia malalamiko chini ya kanuni ndogo ya (1) na kwa mujibu wa kanuni zilizotengenezwa chini ya shria kwa dhumuni hilo.

(3) Pale ambapo mteja hajaridhishwa na uamuzi wa mtoa huduma ndogo za fedha, malalamiko hayo yanaweza kuwasilishwa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(4) Malalamiko ya mteja hayatawasilishwa kwa Waziri isipokuwa pale ambapo malalamiko hayo yameshughulikiwa kwa utaratibu ulioainishwa kwenye Kanuni hizi au malalamiko hayo yanahusu masuala ya sera ambayo yanahijaji Waziri kuingilia kati.

26. Mtu ye yote ambaye atakiuka masharti ya Kanuni hizi pale ambapo adhabu mahsusii haijaainishwa atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atapewa adhabu kama ilivyoainishwa chin ya Sheria.

Makosa
na adhabu

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chin ya kanuni ya 6(2)(g))

TAARIFA ZA VIPINDI MBALIMBALI

SEHEMU A: IDADI YA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
1.	DARAJA LA 2					
2.	DARAJA LA 3					
3.	DARAJA LA 4					

SEHEMU B: IDADI YA WAHAMASISHAJI WA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
1.	DARAJA LA 2					
2.	DARAJA LA 3					
3.	DARAJA LA 4					

SEHEMU C: IDADI YA MIKOPO ILIYOTOLEWA KWA VIPINDI VYA ROBO MWAKA

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	KIPENGELE	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
1.	DARAJA LA 2	Idadi ya mikopo iliyotolewa kwa wanaume					
		Idadi ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake					
2.	DARAJA LA 3	Idadi ya mikopo iliyotolewa kwa wanaume					
		Idadi ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake					
3.	DARAJA LA 4	Idadi ya mikopo iliyotolewa kwa wanaume					

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	KIPENGELE	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
3.	DARAJA LA 4	Idadi ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake					

SEHEMU D: THAMANI YA MIKOPO ILIYOTOLEWA KWA VIPINDI VYA ROBO MWAKA

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	KIPENGELE	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
1.	DARAJA LA 2	Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanaume					
		Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake					
2.	DARAJA LA 3	Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanaume					
		Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake					
3.	DARAJA LA 4	Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanaume					
		Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake					

SEHEMU E: KIASI CHAAKIBA KWA VIPINDI VYA ROBO MWAKA

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	KIPENGELE	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
1.	DARAJA LA 2	Kiasi cha akiba kwa wanaume					
		Kiasi cha akiba kwa wanawake					
2.	DARAJA LA 3	Kiasi cha akiba kwa wanaume					

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	KIPENGELE	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
		Kiasi cha akiba kwa wanawake					
2.	DARAJA LA 3	Kiasi cha akiba kwa wanaume					
		Kiasi cha akiba kwa wanawake					
3.	DARAJA LA 4	Kiasi cha akiba kwa wanaume					
		Kiasi cha akiba kwa wanawake					

SEHEMU F: MIKOPO CHECHEFU

Na.	DARAJA LA WATOA HUDUMA	KIPENGELE	ROBO YA KWANZA YA MWAKA	ROBO YA PILI YA MWAKA	ROBO YA TATU YA MWAKA	ROBO YA NNE YA MWAKA	MWAKA
1.	DARAJA LA 2	Idadi ya mikopo isiyorejeshwa					
		Jumla ya kiasi cha mikopo kisichorejeshwa					
2.	DARAJA LA 3	Idadi ya mikopo isiyorejeshwa					
		Jumla ya kiasi cha mikopo kisichorejeshwa					
3.	DARAJA LA 4	Idadi ya mikopo isiyorejeshwa					
		Jumla ya kiasi cha mikopo kisichorejeshwa					

SEHEMU G: KIWANGO CHARIBA KINACHOTOZWA

Na.	Daraja	Mkopo	Akiba
1.	Daraja la 2		N/A
2.	Daraja la 3		
3.	Daraja la 4		

SEHEMU H: CHANGAMOTO ZINAZOKABILI KILA DARAJA KATIKA BIASHARA YA HUDUMANDOGO ZA FEDHA (KISHERIA, KISERA NA KIUTENDAJI)

.....

.....

.....

SEHEMU I: MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUCHUKUAILI KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO

.....

.....

.....

Imetolewa na:

(Jina la Mratibu)

Saini:

Tarehe:

—————

JEDWALI LA PILI

—————

(Limeandaliwa chini ya kanuni ya 15(3))

—————

FOMU YA MAOMBI YA USAJILI WA MHAMASISHAJI

1. Jina la mwombaji:

.....

2. Usajili wa mwombaji:

(a) Namba ya usajili:

(b) Tarehe ya usajili:

(c) Mamlaka ya usajili:

(d) Mahali ofisi ilipo:

3. Anwani ya makao makuu ya ofisi: L. R. Na.....

Mtaa Kata Wilaya

Mkoa

Jengo:

.....

Eneo unalotarajia kufanyia shughuli

4. Anwani ya posta

Namba ya Posta

Namba ya simu

Namba ya aina ya kitambulisho

Barua pepe

5. Sehemu alizowahi kufanya biashara nchini Tanzania na idadi ya miaka kwa kila biashara

